**Higher School Certificate (HSC) minimum standard**

Information for parents and carers

# Kiwango cha chini cha Cheti Cha Shule ya Juu (HSC)

## Habari kwa wazazi na walezi

Wazazi na walezi wapendwa,

Kuanzishwa kwa sera ya kiwango cha chini cha Cheti Cha Shule ya Juu (HSC) na Mamlaka ya Viwango vya Elimu ya NSW (NSW Education Standards Authority (NESA)) inamaanisha wanafunzi katika NSW wanahitaji kuonyesha kiwango cha chini cha kusoma, kuandika na kuhesabu ili kupokea Cheti chao cha Shule ya Juu (HSC).

Wanafunzi watafanya mitihani ya kiwango cha chini cha HSC katika nyanja tatu za kusoma, kuandika, na kuhesabu. Kila mtihani wa mtandaoni una urefu wa dakika 45 na umeundwa kama ifuatavyo:

- mtihani wa chaguo nyingi kwa kusoma
- mtihani wa chaguo wa kuhesabu; na
- mtihani wa kuandika (hadi maneno 500) kulingana na kisituo kilichoandikwa au ya kuona.

Wanafunzi wanahitaji kufikia Kiwango cha 3 au cha 4 katika vikoa vyote vitatu vya mitihani ili kufikia kiwango cha chini cha HSC. Hii ina maana kwamba wanafunzi wanaoonyesha kiwango wana stadi za kimsingi za utendaji zinazotumiwa katika maisha ya kila siku, kwa kazi na masomo zaidi.

Wanafunzi wana fursa nyingi kila mwaka za kufanya mitihani hiyo mtandaoni, kuanzia Mwaka wa 10 hadi mwisho wa Mwaka wa 12. Kuna muda wa kusuburi kati ya kujaribu tena kila mtihani.

Wanafunzi watasaidiwa na shule kufikia kiwango cha chini cha HSC. Kuna majaribio ya mazoezi yanayopatikana shuleni na maswali ya onyesho mtandaoni kwenye tovuti ya NESA: https://educationstandards.nsw.edu.au/wps/portal/nesa/11-12/hsc/hsc-minimum-standard/online-tests

Tafadhali wasiliana na shule ikiwa ungependa habari zaidi.

Iwapo unaamini kuwa mtoto wako ana mahitaji ya ziada na atastahiki masharti ya ziada kwa ajili ya mitihani ya kiwango cha chini cha HSC, tafadhali mpigie simu mtu anayewasiliana naye shuleni aliyeonyeshwa hapa chini:

Jina la mtu wa kuwasiliana naye shuleni

Nambari ya simu ya mtu wa shule

Wako mwaminifu

Mkuu wa shule

Jina la shule

### Huduma la Mkalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji mkalimani ili kukusaidia kuwasiliana na shule, tafadhali pigia simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa nambari 131 450 na uombe mkalimani katika lugha yako. Mwambie opereta nambari ya simu unayotaka kupiga simu na opereta atapata laini ya muda ili kukusaidia kwa mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.